# TAARIFA KUHUSU UCHAGUZI KWA VIWANGO VYA UPENDELEO

**Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo ni nini?**

Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo (RCV) ni mbinu ya uchaguzi inayowapa wapiga kura chaguo la kuwapa madaraja wagombea kulingana na upendeleo wao (chaguo la kwanza, la pili, la tatu, na kadhalika). Uwekaji viwango kwa wagombea ni tofauti na kuchagua mgombea mmoja tu au kile kinachojulikana kama upigaji wa kura nyingi. Ikiwa mgombea atapata zaidi ya asilimia 50 ya chaguo za kwanza, mgombea huyo anashinda, kama ilivyo katika uchaguzi mwingine wowote. Hata hivyo, ikiwa hakuna mshindi wa kura nyingi baada ya kuhesabu chaguo za kwanza, uchaguzi huamuliwa kwa kurudiwa mara moja. Mgombea aliye na kura chache zaidi huondolewa, na wapiga kura waliompa kiwango mgombea huyo kama chaguo lao la kwanza kura zao zitatumika kwa chaguo lao linalofuata. Mchakato huu utaendelea hadi mgombea atakaposhinda kwa zaidi ya asilimia 50 ya kura.

Kwa taswira ya jinsi kura zinavyohesabiwa katika raundi husika, tembelea NYC Votes.

**Kwa nini tunatumia Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo?**

Mnamo Machi 2021, wakazi wa Burlington walipiga kura kutumia Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo kwa Madiwani wa Jiji. Ilipita kwa uungwaji mkono wa asilimia 64.

**Je, ni Chaguzi zipi zitatumia Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo?**

Burlington itatumia Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo wakati wa kuwachagua Madiwani wa Jiji tu.

**Je, nawekaje alama kwenye kura yangu?**

Kwenye Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo, wapiga kura huweka alama kwenye kura zao kulingana na upendeleo wao – chaguo la 1, chaguo la 2, la 3, na kadhalika.

1. Teua mgombea ambaye ndiyo chaguo lako la kwanza kwa kujaza kabisa duara dufu karibu na jina la mgombea husika katika safu wima ya CHAGUO LA KWANZA.

2. Iwapo una mgombea wa chaguo la pili, jaza kabisa duara dufu lililopo karibu na jina la mgombea huyo katika safu wima ya CHAGUO LA PILI.

3. Iwapo una mgombea wa chaguo la tatu, jaza kabisa duara dufu karibu na jina la mgombea huyo katika safu wima ya CHAGUO LA TATU.

4. Unaweza kuendelea kuchagua kwa kuwapa madaraja wagombea hadi umalize nafasi zinazokubalika au wagombea unaopendelea waishe.

**Mambo muhimu kuhusu kuweka alama kwa usahihi kwenye kura ya Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo:**

- Weka alama kwenye chaguo moja pekee kwa kila safu wima.
- Weka alama kwenye chaguo moja pekee kwa kila mgombea.
- Usiruke daraja. Kwa mfano, usijaze chaguo la 1 na la 3 bila kujaza chaguo la pili.
- Unaweza kuchagua wagombea wachache kwa viwango vya upendeleo kadri unavyopenda.
- Unaweza kuchagua wagombea wengi kwa viwango vya upendeleo kadri unavyopenda.

Nyenzo: *Kituo cha Nyenzo za Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo,* https://www.rcvresources.org/.

- **MFANO WA 1:**

**Kura iliyowekwa alama kwa usahihi, ambayo mpiga kura ameonyesha chaguo la 1, la 2 na la 3.**

| **WAGOMBEA** | CHAGUO LA 1 | CHAGUO LA 2 | CHAGUO LA 3 |
|---|---|---|---|
| stroberi | ○ | ○ | ● |
| chokoleti | ● | ○ | ○ |
| vanila | ○ | ● | ○ |

**MFANO WA 2:**

**Nafasi ya 2 iliyopigiwa kura kupita kiasi ambapo chaguo la 1 limewekwa alama kwa usahihi, wagombea wawili wamewekewa alama kwa chaguo la 2, chaguo la 3 halijawekwa alama.**

Jinsi kura ya mpiga kura huyu itakavyohesabiwa:

- Chaguo la kwanza litahesabiwa.
- Kura ya chaguo la pili haitahesabiwa – nia ya mpiga kura haiwezi kubainishwa kwa sababu safu wima hii imepigiwa kura nyingi kupita kiasi.

| **WAGOMBEA** | CHAGUO LA 1 | CHAGUO LA 2 | CHAGUO LA 3 |
|---|---|---|---|
| stroberi | ● | ○ | ○ |
| chokoleti | ○ | ● | ○ |
| vanila | ○ | ● | ○ |

**MFANO WA 3:**

**Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo uliorudiwa ambapo mgombea mmoja amewekewa alama kwa chaguo za 1, 2 na 3.**

Jinsi kura ya mpiga kura huyu itakavyohesabiwa:

- Chaguo la kwanza litahesabiwa.
- Iwapo mgombea wa chaguo la kwanza ataondolewa, chaguo la pili na la tatu haliwezi kuzingatiwa, kwa kuwa zimerudiwa.

| **WAGOMBEA** | CHAGUO LA 1 | CHAGUO LA 2 | CHAGUO LA 3 |
|---|---|---|---|
| stroberi | ● | ● | ● |
| chokoleti | ○ | ○ | ○ |
| vanila | ○ | ○ | ○ |

Nyenzo: *Kituo cha Nyenzo za Uchaguzi kwa Viwango vya Upendeleo,* https://www.rcvresources.org/.